

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU**



TAARIFA KWA UMMA

**KUHUSU TAARIFA YA UPOTOSHAJI KUHUSIANA NA NAFASI ZA
KAZI YA UKUSANYAJI USHURU WA MAEGESHO YA VYOMBO VYA
MOTO**

1. Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu inapenda kuujulisha UMMA wa Watanzania kuwa kumekuwepo na taarifa zilizoza taharuki baina ya wananchi kupitia mitandao ya kijamii ikiwemo "Whatsapp" kuhusu nafasi ya kazi ya kukusanya ushuru wa maegesho ya vyombo vya moto (Magari, Bajaji na Pikipiki) katika Mikoa ya Mwanza, Mbeya, Arusha, Dodoma na Dar Es Salaam. Aidha, katika tangazo hilo imeelezwa kuwa kazi hiyo itakuwa ya mkataba wa miezi sita (6) na mshahara utakuwa kuanzia Shilingi 300,000/= kwa mwezi.
2. Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu inakanusha kuhusu tangazo hilo na kueleza UMMA kuwa wapuuze taarifa hizo kwa kuwa hazina ukweli wowote na wala hazijatolewa na Ofisi hii, ambayo ndio yenye dhamana ya kusimamia masuala ya Kazi.
3. Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu inawataka watu wanaoeneza taarifa hizo za uongo kuacha upotoshaji huo mara moja. Aidha, hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao endapo watabainika kukaidi maelekezo haya.

**IMETOLEWA NA:
KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI
28 DISEMBA, 2020**